
# Barua kwa Mpenzi

Comp: Wachira Sammy

***Imba kwa mwendo wa Rhumba***

Umerekodiwa na: St Gregory the great Choir
Malindi Cathedral




Copyright © <2015> by samirmuriuki@gmail.com +254720883008
All Rights Reserved




1. Barua nimekuandikia mpenzi tulia uisome, miaka sasainasogea sina budi kukuarifia, inatupasa kuliwazia jambo hili la kufunga ndoa, twendekanisani tukapate Barakazake Mungu mwenyezi.

***Nimeamua ni wewe pekee mpenzi wangu sina mwengine.***
***Nimekubali kukupokea mpenzi wangu nivishe pete.***
***Mpenzi njoo tuandamane, pingu za maisha tuzifunge, Pokea pete hii ni ishara***
***Ya upendo wangu kwako wewe***
***(Kwa jina la Baba na la mwana Roho mtakatifu Amina) x2***

2. Nikitazama jinsi wenzangu wanavyojongea altarini, moyo wangu unahuzunika ninapowaziajambo hili, inatupasa kuishiriki sakramenti hii ya upendo, tusiwe tuwa kushangilia kwenye harusi za wenzi wetu.

3. Ni wengi wamenitamania niweze fungua roho kwao, najua kwako ni vilevile wengi wanakumezea mate, wakati sasa umeshafika mpenzi njoo tuweke wazi, ulimwengu wote utambue mimi nawe kweli twapendana.

4. Mungu amekwisha tuteuwa tuweze kuwa mwili mmoja, Alichokiunganisha Mungu mwanadamu asitenganishe, wewe ni ubavu utokao kwenye ubavu wangu mwenyewe tuombee Mungu atubariki tuweze kuishi kwa upendo.